**NIA ZA SALA ZA BABA MTAKATIFU**
**ZILIZOKABIDHIWA KWA MTANDAO WAKE WA SALA**
**KWA MWAKA 2026**

## JANUARI

**Kwa ajili ya kusali kwa kutumia Neno la Mungu**
Tuombe ili kusali kwa kutumia Neno la Mungu kuwe kirutubisho kwa maisha yetu na chanzo cha matumaini katika jumuiya zetu, na msaada wa kujenga Kanisa la kidugu na kimisionari zaidi.

## FEBRUARI

**Kwa ajili ya watoto wenye maradhi yasiyotibika.**
Tusali ili watoto walio na magonjwa yasiotibika na familia zao, wapate huduma muhimu za kitabibu, bila kupoteza nguvu na matumaini.

## MACHI

**Kwa upokonyaji silaha na amani**
Tusali ili mataifa yaelekee upande wa kukomesha matumizi ya silaha, hasa silaha za nyuklia, na kwamba viongozi wa dunia wachague njia ya mazungumzo na diplomasia badala ya matumizi ya nguvu.

## APRILI

**Kwa ajili ya mapadre wenye changamoto.**
Tusali kuwaombea makasisi wanaopitia nyakati ngumu katika miito yao, wapate msaada wanaohitaji na jumuiya za watu ziwasaidie kwa kuelewa wanayopitia na kuwaombea.

## MEI

**Kwamba kila mtu awe na chakula**
Tusali ili kila mtu, kuanzia wazalishaji wakubwa hadi wanunuzi wadogo wa chakula, wawe makini kukwepa ufujaji wa chakula, na kuhakikisha kuwa kila mtu anaweza kupata chakula bora.

## JUNI

**Kwa ajili ya umuhimu wa michezo**
Tusali ili michezo iwe chombo cha amani, maonano na mazungumzo baina ya tamaduni na mataifa, na kujenga maadili ya heshima, mshikamano na makuzi binafsi

## JULAI

**Kwa ajili ya heshima ya maisha ya binadamu**
Tusali kwa ajili ya heshima na ulinzi wa maisha ya mwanadamu katika hatua zake zote, tukiyatambua maisha kama zawadi ya Mungu.

## AGOSTI

**Kwa ajili ya uinjilishaji mjini**
Tusali ili kwamba katika miji mikubwa iliyogubikwa na kutotambuana na upweke wa watu, tuweze kupata njia mpya za kutangaza Injili, na kubuni njia mpya za kujenga jamii ya watu.

## SEPTEMBA

**Kwa ajili ya utunzaji wa maji.**
Tusali kwa ajili ya usimamizi endelevu na wa haki wa maji iliyo rasilimali muhimu, ili kila mtu awe na nafasi sawa ya kupata maji.

## OKTOBA

**Kwa ajili ya utume wa afya ya akili.**
Tusali kuomba ili utume wa afya ya akili uanzishwe katika Kanisa zima, ili kusaidia kuondoa unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya walio na maradhi ya akili.

## NOVEMBA

**Kwa matumizi sahihi ya mali.**
Tusali kuombea matumizi mazuri ya mali, kwamba tusiangukie kishawishi cha ubinafsi, bali mali daima itumike kwa manufaa ya wote na kwa usaidizi wa wale waliopungukiwa nayo.

## DESEMBA

**Kwa ajili ya familia zenye mzazi mmoja.**
Tusali kuziombea familia zisizo na baba au mama, ili kwamba zipate usaidizi na ushirikiano katika Kanisa, na kuimarishwa katika Imani zipitiapo nyakati ngumu

Papa Leo XIV

Vatikan, Julai 1, 2025
*Lugha ya Uandishil: Kiitaliano*